

**TAARIFA YA MAADHIMISHO YA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA  
YALIYOFANYIKA KIMKOA KATIKA VIWANJA VYA MNAZI MMOJA,  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA 16/6/2011**

**1.0 Utangulizi**

Siku ya siku ya Mtoto wa Afrika huadhimishwa tarehe 16, Juni ya kila mwaka. Siku hii inaadhimishwa kwa Azimio la nchi 51 wanachama wa uliokuwa Umoja wa Nchi huru za Afrika (OAU) kwa ajili ya kukumbuka mauaji ya kinyama waliofanyiwa watoto wa kitongoji cha Soweto nchini Afrika ya Kusini mnamo mwaka 1976. Hapa nchini kuna utaratibu wa kuazimisha Kitaifa kila baada ya miaka mitano, mwaka huu maadhimisho yamefanyika Kimkoa. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam maadhimisho haya yalifanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Hii ni kutokana na utaratibu tuliojiwekea wa kuadhimisha kwa kila mwaka kwa awamu katika Halmashauri za Manispaa za Mkoa wa Dar es salaam.

**2.0 Lengo la Maadhimisho**

Siku hii huadhimishwa kwa lengo la kukumbuka mauaji ya kinyama waliofanyiwa watoto nchini Afrika ya Kusini wakati wakidai haki zao za msingi, pia kuwakumbusha wazazi/walezi na jamii kwa ujumla juu ya haki na wajibu wa jamii katika kuwalea watoto. Aidha, hutoa nafasi ya kuwakumbusha watoto haki na wajibu wao kama watoto katika Taifa.

**3.0 Kauli mbiu**

Kauli mbiu ya mwaka huu (2011) inasema ***"Tuungane Pamoja Kuchukua Hatua za Haraka Kushughulikia Tatizo la Watoto Wanaoishi Mitaani"***. Ikiwa na maana ya kukumbusha umuhimu wa wazazi, walezi wadau wote katika kushughulikia tatizo la watoto wanaoishi mitaani na kwamba watoto hawa ni wetu na ndio msingi mkubwa wa kuleta maendeleo ya nchi hii kwa siku za baadae. Hivyo basi, jamii tunao wajibu kipekee wa kumuandaa mtoto wa taifa hili ili awe raia mwema.

**4.0 Yaliyojitokeza**

- Risala ya watoto
- Hotuba ya Mgeni rasmi
- Vikundi vya burudani
- Mgeni rasmi kutembelea mabanda

**4.1 Risala ya watoto**

Watoto walipata nafasi ya kusoma risala mbele ya Mgeni rasmi, wazazi, walezi na wadau mbalimbali ambayo iliwasilishwa kwa niaba ya watoto wenzao wa Mkoa wa Dar es salaam. Katika risala yao watoto walimshukuru mgeni rasmi kwa

kukubali kuungana nao katika maadhimisho hayo. Risala hiyo ilitoa ujumbe mbalimbali ikiwa ni pamoja na;-

- Jamii kuweka utaratibu wa kuwahudumia watoto wote bila kubagua
- Serikali iangalie namna ya kuondoa umaskini wa kipato katika ngazi ya familia
- Baadhi ya watu katika jamii waache tamaa ya kuchukua mali na kuwaacha watoto wakihangaika mitaani pindi wazazi wao wanapofariki dunia.

Pia, risala ilibainisha vyanzo vya watoto kwenda kuishi mitaani kama vile, kutopata upendo kutoka kwa wazazi na walezi, matatizo mimba za utotoni, utoro shuleni na tamaa. Hivyo jamii na watoto wanapaswa wafahamu haki na wajibu wao.

#### **4.2 Hotuba ya Mgeni rasmi**

Hotuba ya Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Said Meck Sadick katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ilisomwa na Ndugu E. Ntandu Katibu Tawala Msaidizi Idara ya Mipango na Uratibu aliyemwakilisha Kaimu Mkuu wa Mkoa katika maadhimisho hayo. Katika hotuba yake Mgeni rasmi aliwashukuru Wataalamu wa Sekretarieti na Halmashauri za Manispaa katika kuandaa siku hiyo. Aidha, alitoa Shukrani za dhati kwa Shirika la AMREF, Benki ya CRDB, Benki ya Wananchi, Shirika lisilo la kiserikali la Dar Urban Plan na Wadau wengine wote kwa kutambua mchango wao katika kuadhimisha siku ya Mtoto wa Afrika ndani ya Mkoa wetu. Pia alisisitiza kwamba kwa mwaka ujao wazazi na walezi wengi wahamasishwe ili waungane pamoja na watoto wao katika kuadhimisha siku hiyo ili ujumbe unapotolewa uweze kuwafikia.

Mgeni rasmi alitoa wito kwa jamii itimize wajibu wake kama kauli mbiu ya mwaka huu unavyotutaka na kuaahidi kwamba Mkoa utaendelea kutoa fursa kwa watoto ili kuweza kutoa maoni yao kwa Maendeleo ya Taifa na kuwachukua hatua kali za kisheria wale wote wanaoendeleza ukatili dhidi ya watoto.

#### **4.3 Vikundi vya burudani.**

Watoto walipata nafasi ya kuonesha burudani mbalimbali kwa Mgeni rasmi na watu wote waliofika katika viwanja vya Mnazi Mmoja. Burudani hizo zilikuwa ni pamoja na Ngoma ya mganda, kwaya na maigizo zikiwa zimebeba ujumbe mbalimbali kama vile, ajira za watoto zikomeshe na wazazi na walezi wapelekwe watoto shuleni kwani uridhi pekee wa wazazi kwa watoto ni elimu, jamii iwalee na kuwatunza watoto. Aidha, Serikali iendeele kutoa elimu kwa jamii juu ya haki na wajibu wa watoto na jamii.

#### **4.4 Mgeni rasmi kutembelea mabanda**

Mgeni rasmi alipata nafasi ya kutembelea mabanda ambayo yalishehenezwa na kazi mbalimbali za watoto zikiwemo; - picha za kuchora, vifaa vya kufinyanga kwa udongo (kinu na kibao cha kusukumia chapati), bangili za wanawake za kuvaa mikononi ambazo hutengenezwa na watoto wenye ulemavu wa macho.

#### **5 Hitimisho**

Kila mmoja wetu awajibike kwa nafasi aliyonayo katika kuhakikisha tatizo la watoto wanaoishi mitaani linatoweka na hatimaye kuwa na Taifa endelevu lenye kutekeleza na kusimamia misingi ya haki na wajibu kwa watoto.